**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TAARIFA YA MAFANIKIO KATIKA KIPINDI CHA SIKU 100 BAADA YA SERIKALI KUINGIA MADARAKANI

**IMEANDALIWA NA:**

***OFISI YA WAZIRI MKUU***

***(SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU)***

***FEBRUARI, 2026***

# YALIYOMO

YALIYOMO ..... i
SURA YA KWANZA ..... 1
1. UTANGULIZI ..... 1
SURA YA PILI ..... 4
2. FEDHA, MIPANGO NA UWEKEZAJI ..... 4
2.1. FEDHA ..... 4
2.2. MIPANGO NA UWEKEZAJI ..... 5
SURA YA TATU ..... 7
3. SEKTA ZA HUDUMA YA JAMII ..... 7
3.1. AFYA ..... 7
3.2. ELIMU ..... 8
3.3. MAJI ..... 10
SURA YA NNE ..... 12
4. SEKTA ZA UZALISHAJI ..... 12
4.1. KILIMO ..... 12
4.2. MIFUGO NA UVUVI ..... 13
4.3. VIWANDA NA BIASHARA ..... 14
4.4. MADINI ..... 15
4.5. MALIASILI NA UTALII ..... 16
4.6. ARDHI ..... 17
4.7. NISHATI ..... 19
SURA YA TANO ..... 20
5. UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO ..... 20
5.1. UJENZI ..... 20
5.2. UCHUKUZI ..... 21
5.3. MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI ..... 22
SURA YA SITA ..... 24
6. ULINZI NA USALAMA ..... 24
SURA YA SABA ..... 25
7. UTUMISHI NA UTAWALA BORA ..... 25
7.1. UTUMISHI ..... 25

7.2. UTAWALA BORA ........................................................................................ 25
SURA YA NANE ........................................................................................................ 26
8. USHIRIKANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA .................................................. 26
SURA YA TISA ......................................................................................................... 27
9. KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO ........................................................................... 27
SURA YA KUMI ........................................................................................................ 28
10. URATIBU WA MASUALA MBALIMBALI ........................................................ 28
10.1. MAZINGIRA ........................................................................................................ 28
10.2. MAENDELEO YA JAMII ................................................................................... 28
10.3. MAENDELEO YA VIJANA ................................................................................ 31
10.4. UJENZI NA UENDELEZAJI MJI WA SERIKALI .......... **Error! Bookmark not defined.**
10.5. KUDHIBITI UZALISHAJI NA USAMBAZAJI WA DAWA ZA KULEVYA .. 31
10.6. MAPAMBANO DHIDI YA VVU NA UKIMWI ............................................. 32
10.7. URATIBU WA SHUGHULI ZA MAAFA ........................................................ 32
10.8. HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO ....................................... 33
SURA YA KUMI NA MOJA ...................................................................................... 34
11. HITIMISHO ......................................................................................................... 34

## SURA YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 zilizofanyika kuanzia Agosti hadi Oktoba, 2025 alitoa ahadi mbalimbali kwa wananchi ikiwemo ahadi zitakazotekelezwa ndani ya siku 100 baada ya kuchaguliwa na kuingia madarakani katika kipindi cha pili cha awamu ya sita. Baada ya kushinda uchaguzi na kuingia madarakani tarehe 03 Novemba, 2025 aliunda Serikali na kuanza utekelezaji wa ahadi ikiwemo kuimarisha utoaji wa huduma za afya, elimu, maji; kurasimisha sekta isiyo rasmi; kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo, za kati na uendeshaji wa kampuni changa; na kuunda Tume ya Kuanzisha Mazungumzo ya Maridhiano na Upatanishi pamoja na kuandaa mazingira ya kuanza kwa mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Vilevile, Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania wakati akifungua rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025 alisisitiza kuanza utekelezaji wa ahadi hizo.

Ahadi hizo zimetekelezwa kwa mafanikio makubwa kupitia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa chini ya kauli mbiu ya ***Kazi na Utu, Tunasonga Mbele***. Baadhi ya mafanikio makubwa yamepatikana katika sekta za afya, elimu na maji. Kwa upande wa sekta ya afya, Serikali imewezesha kuanza kutumika kwa huduma ya Bima ya Afya kwa Wote kwa awamu ya kwanza ya wananchi wasio na uwezo watakaogharamiwa bima ya afya na Serikali; kuanza kutumika kwa utaratibu wa kugharamia magonjwa sugu (Saratani, Figo, Moyo, Kisukari na Mifupa) kwa watu wasio na uwezo; na kuondoa zuio la kuchukua miili ya marehemu katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini kwa kigezo cha kutokulipia gharama za matibabu na madeni.

Vilevile, kwa upande wa sekta ya elimu, Serikali imeandaa na kuanza kutekeleza Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu wenye kauli mbiu ya '*Mtoto Asome, Aandike na Ahesabu bila shida*' unaolenga kuongeza ubora wa elimu ya msingi na mbinu bora za kufundishia; na kuandaa Mpango wa pamoja kati ya waajiri, Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo Vikuu unaolenga kuwajengea uwezo wa ubunifu na ujasiriamali wanafunzi ili kuwawezesha kujiajiri. Aidha, kwa upande wa sekta ya maji, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya dhana ya Mtandao wa Taifa wa Kusambaza

Maji (National Water Grid) katoka kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa na mito mikubwa.

Vilevile, Serikali imeajiri watumishi wa sekta ya Afya 5,000 na sekta ya elimu 7,000. Watumishi hao wameongeza hali ya utoaji wa huduma za afya pamoja na kupunguza upungufu wa walimu wa sayansi katika maeneo mbalimbali nchini. Katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kujiajiri kwa kutoa fedha za mitaji shilingi bilioni 200 zitakazotolewa kwa vijana wa maeneo mbalimbali nchini kwa kuzingatia shughuli wanazotekeleza. Kutolewa kwa fedha hizo kutaongeza uzalishaji wa ajira na hivyo kuwezesha vijana kuongeza kipato na kukuza uchumi wa nchi.

Katika suala la maridhiano na mchakato wa mabadiliko ya Katiba, Serikali imeanza utekelezaji kwa kuunda Tume Huru ya Uchunguzi wa matukio ya uvunjifu wa amani yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Matokeo ya uchunguzi huo yatawezesha kuanzisha mazungumzo ya maridhiano na upatanishi na kuanza kwa mchakato wa mabadiliko ya Katiba.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa ahadi za siku 100, mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania ambapo jumla ya shilingi trilioni 6.99 zilikusanywa kati ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 6.86 sawa na asilimia 101.89 katika kipindi cha Novemba na Desemba, 2025. Vilevile, mfumuko wa bei umedhibitiwa na kufikia asilimia 3.6 Desemba, 2025 na hivyo kuendelea kubaki ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0. Aidha, Serikali imeandaa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2050 (LTPP 2050) unaoelekeza kuhusu utekelezaji wa Dira 2050 kupitia mipango ya miaka mitano (*Five Year Development Plans-FYDPs*).

Kwa upande wa usafiri na usafirishaji, Serikali imezindua Meli ya New MV Mwanza inayotoa huduma za usafiri wa abiria na mizigo katika Ziwa Victoria; kukamilisha ujenzi wa Jengo la Viongozi (Presidential Pavillion) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere – (Terminal I) lenye uwezo wa kuhudumia wakuu wa nchi watano (5) kwa wakati mmoja; na kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Kemondo katika Ziwa Victoria ambayo ni kituo cha usafirishaji katika maeneo ya Bukoba, Mwanza na bandari za Uganda.

Taarifa hii imeainisha mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya siku 100 za Serikali ya Awamu ya Sita Kipindi cha Pili katika Sura kumi na moja (11). Sura ya Kwanza ni utangulizi; Sura ya Pili ni hali fedha, mipango na uwekezaji; Sura ya tatu ni sekta za huduma ya jamii; Sura ya Nne ni sekta za uzalishaji; Sura ya Tano ni ujenzi, uchukuzi na mawasiliano; Sura ya Sita ni ulinzi na usalama; Sura ya Saba ni utumishi na utawala bora; Sura ya Nane ni ushirikiano wa kikanda na kimataifa; Sura ya Tisa ni Kazi, Ajira na Mahusiano; Sura ya Kumi ni uratibu wa masuala mbalimbali; na Sura ya Kumi na Moja ni hitimisho.

## SURA YA PILI

## 2. FEDHA, MIPANGO NA UWEKEZAJI

### 2.1. FEDHA

Sekta ya fedha imeendelea kukua kwa kasi na kuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya uchumi nchini, ikichochewa na ongezeko la huduma za kifedha za kidijitali, upanuzi wa huduma za benki vijijini na kuimarika kwa ufikiaji wa huduma za kifedha kwa wananchi. Mafanikio mengine yaliyopatikana katika siku 100 ni kama ifuatavyo:

i. Kuongezeka kwa mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania ambapo kwa kipindi cha Novemba na Desemba, 2025 jumla ya shilingi trilioni 6.99 zilikusanywa kati ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 6.86 sawa na asilimia 101.89. Makusanyo hayo yamewezesha Serikali kugharamia huduma za jamii na miradi ya maendeleo ikiwemo afya, elimu, maji na miundombinu bila kuongeza mzigo wa kodi kwa wananchi;

ii. Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei ndani ya viwango vinavyokubalika ambapo katika kipindi cha Novemba 2025, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.4 na kwa Desemba 2025 ulifikia asilimia 3.6. Viwango hivyo, vipo ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0, vigezo vya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (usiozidi asilimia 8.0) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (wigo wa asilimia 3.0 hadi 7.0). Udhibiti huo umeweka mazingira tulivu ya uchumi kwa wafanyabiashara na wawekezaji, hivyo kuchangia ustawi wa jamii kwa ujumla;

iii. Kuendelea kuimarika kwa akiba ya fedha za kigeni na kufikia dola za Marekani milioni 6,329 Desemba, 2025, kiwango ambacho kinatosha kugharamia mahitaji ya miezi 4.9 ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje. Kiwango hicho kimezidi vigezo vya kitaifa (kuanzia miezi 4) na vile vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuanzia miezi 4.5. Kuimarika kwa akiba ya fedha za kigeni kumeihakikishia nchi uwezo wa kuagiza bidhaa muhimu kama mafuta, vipuri, dawa na pembejeo za uzalishaji na hivyo kuchangia upatikanaji endelevu wa bidhaa na huduma muhimu kwa wananchi;

iv. Kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nje ya nchi kufikia dola za Marekani milioni 609.7 Desemba, 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 657.5 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Ufanisi huo ulitokana na utendaji mzuri wa mauzo ya nje ya bidhaa na huduma, sambamba na ongezeko la wastani la uagizaji wa bidhaa, hususan pembejeo za uzalishaji na shughuli za uwekezaji;

v. Kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi kufikia dola za Marekani milioni 10,002.8 katika kipindi kilichoishia Desemba 2025, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,376.6 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024. Ongezeko hilo limechangiwa na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani, tumbaku, korosho na kahawa nje ya nchi. Mafanikio hayo yameongeza mapato ya fedha za kigeni, kukuza uzalishaji wa ndani, kuongeza ajira, hususan katika sekta za kilimo, viwanda na madini pamoja na kuchangia ukuaji wa uchumi unaowanufaisha wananchi;

vi. Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya dhahabu nje ya nchi kutoka dola za Marekani milioni 3,320.8 Novemba 2024 hadi kufikia dola za Marekani milioni 4,719.8 Novemba 2025 sawa na asilimia 42.1. Ongezeko hilo lilitokana na kupanda kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia sambamba na kuongezeka kwa uzalishaji;

vii. Kuanzishwa kwa Hatifungani ya TCB Stawi (TCB Stawi Bond) mnamo Novemba 2025. Hatifungani hiyo ilitolewa chini ya mpango wa Hatifungani za Muda wa Kati wenye thamani ya shilingi bilioni 150, ambapo toleo la awali lilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 50, na iliweza kuvutia wawekezaji kwa kiwango kikubwa hali iliyosababisha kuandikishwa kupita kiasi (*oversubscription*) na kukusanya shilingi bilioni 140. Hatua hii imeongeza fursa za uwekezaji kwa wananchi na taasisi za ndani, pamoja na kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa biashara ndogo na za kati; na

viii. Kukamilisha ujenzi wa Mfumo wa Wastaafu wanaolipwa pensheni na Serikali ili kuhakiki taarifa zao wenyewe. Mfumo huo, umeanza kutumika rasmi tarehe 15 Januari, 2026 ambao umerahisisha na kusogeza huduma karibu na wastaafu kwa kuwapunguzia usumbufu katika kufanya uhakiki wa taarifa zao.

### 2.2. MIPANGO NA UWEKEZAJI

Serikali imeendelea kupanga na kusimamia utekelezaji wa mipango ya kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 iliyoainisha vipaumbele vya Taifa, matumizi ya rasilimali kwa ufanisi, na sekta zenye tija katika uwekezaji na hivyo kukuza fursa za ajira, kuongeza mapato ya Serikali na kuimarisha uchumi wa nchi. Mafanikio yaliyopatikana katika siku 100 ni kama ifuatavyo:

i. Kuandaa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2050 (LTPP 2050) unaoelekeza kuhusu utekelezaji wa Dira inayotekelezwa kupitia mipango ya miaka mitano (*Five Year Development Plans- FYDPs*);

ii. Kuandaa Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 ambao umeweka msingi wa utekelezaji wa Dira 2050;

iii. Kuandaa Mpango wa Pili wa Maboresho ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI II) kwa kuzingatia maono ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Mpango huu unalenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;

iv. Kuanzisha Kituo Maalum cha kuhudumia na kuwezesha wawekezaji vijana (*Youth Investors Resource Centre*) kilichopo Mabibo - Dar es salaam kitakachotoa huduma za mafunzo, uwezeshaji na usaidizi kwa wawekezaji vijana; na

v. Kuanzisha programu maalum ya kuwezesha wawekezaji vijana kubuni na kuanzisha viwanda katika maeneo ya Mikoa ya Dodoma (Nala, ekari 100), Pwani (Kwala, ekari 20 na Bagamoyo, ekari 20), Mara (Bunda, ekari 100) na Ruvuma (Songea, ekari 100).

**SURA YA TATU**

# 3. SEKTA ZA HUDUMA YA JAMII

## 3.1. AFYA

Sekta ya Afya ni nguzo muhimu katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema inayowawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii, hivyo kuongeza uzalishaji, kipato cha mtu mmoja mmoja na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za afya zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuanza kutumika kwa huduma ya Bima ya Afya kwa Wote kwa awamu ya kwanza ya wananchi wasio na uwezo watakaogharamiwa bima ya afya na Serikali kuanzia tarehe 26 Januari, 2026;

ii. Kutoa shilingi bilioni 48.78 kwa ajili ya kuanza kugharamia Bima ya Afya kwa wote kwa awamu ya kwanza kwa wananchi 1,457,602 sawa na kaya 276,004 zisizo na uwezo, wazee 235 na watoto 265 wanaoishi kwenye makazi yanayomilikiwa na Serikali;

iii. Kukamilika kwa Mkakati wa Taifa wa mawasiliano wa Bima ya Afya kwa wote (2025/26-2030/31) unaolenga kuwaelimisha wananchi ili waone umuhimu wa kujiunga na Bima ya Afya;

iv. Kuanza kutumika kwa utaratibu wa kugharamia magonjwa sugu (Saratani, Figo, Mo-yo, Kisukari na Mifupa) kwa wananchi wasio na uwezo kupitia Mfuko wa Kughara-mia Bima ya Afya kwa wananchi wasio na uwezo (*Equity Fund*), ambapo katika awamu ya kwanza ya utekelezaji kiasi cha shilingi bilioni 6.8 kitatumika kugharamia matibabu ya magonjwa sugu na huduma za dharura;

v. Kufanyika kwa Jukwaa la Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi (*Pharmaceutical Production Investment Forum*) tarehe 19 Januari, 2026 lililohudhuriwa na washiriki 536 wakiwemo 36 kutoka nje ya nchi. Jukwaa hilo lilitumika kuelezea fursa za uwekezaji kwenye viwanda vya bidhaa za afya, dhamira ya Serikali katika kujenga Tanzania ya viwanda na kuhamasisha fursa za uwekezaji zilizotangazwa kupitia tangazo la *Call for Expression of Interest (EOI*) linalotarajiwa kufungwa tarehe 2 Machi, *2026;*

vi. Kufufua kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical Industries* (TPI) cha kuzalisha dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI (ARVs), kwa kushirikiana na Sekta Binafisi ambapo Serikali inamiliki asilimia 70 ya hisa. Kiwanda hicho kinatarajiwa kuanza uzalishaji ifikapo mwezi Juni, 2026;

vii. Kuanzisha mfumo wa kidigitali wa *Ongea na Waziri wa Afya* unaolenga kuimarisha uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wananchi katika sekta ya afya kwa kuwapa jukwaa la moja kwa moja kutoa maoni, kero na mapendekezo mbalimbali.

viii. Kuondoa zuio la kuchukua miili ya marehemu katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini kwa kigezo cha kutokulipia gharama za matibabu na madeni. Aidha, uanzishaji wa bima ya afya kwa wote utachangia kulipa gharama za matibabu na kuondoa changamoto hiyo;

ix. Kutoa shilingi bilioni 39.3 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za uzazi na watoto wachanga kwenye vituo vya kutolea huduma za afya 89 ikijumuisha hospitali za wilaya 20, vituo vya afya 19 na zahanati 50;

x. Kuongezeka kwa idadi ya vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni kutoka vituo 523 Oktoba 2025 hadi vituo 578 Januari 2026, ongezeko la vituo hivyo limewezesha kuongezeka kwa asilimia ya wanawake wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya kutoka asilimia 85 Oktoba, 2025 hadi asilimia 87.5 Januari 2026;

xi. Kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa majengo 87 ya huduma za dharura (EMD) na 30 ya wagonjwa mahututi (ICU);

xii. Kukamilika kwa ununuzi na usimikaji wa mitambo 21 ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni katika vituo vya kutolea huduma za afya; na

xiii. Kufunga Mfumo wa Taarifa za Usimamizi na Uendeshaji wa Afya wa Serikali ya Tanzania (GoTHOMIS) katika vituo 7,427 vya kutolea huduma za afya ya msingi.

## 3.2. ELIMU

Serikali imeendelea kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa elimu nchini ili kuzalisha wataalam wenye ujuzi na maarifa ya kujiajiri na kuajiriwa. Mikakati inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 inayolenga kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo unaoweza kumuandaa Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

### 3.2.1. Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu

i. Kukamilika kwa ununuzi na usambazaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vyenye thamani ya shilingi bilioni 5.4 kwa walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi na walimu wenye mahitaji maalum nchini;

ii. Kuchapa na kusambaza vitabu milioni 18 vya ziada ili kuboresha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi na ujifunzaji; na

iii. Kuzinduliwa na kuanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu wenye kauli mbiu ya 'Mtoto Asome, Aandike na Ahesabu bila shida' unaolenga kuongeza ubora wa elimu ya msingi na mbinu bora za kufundishia;

iv. Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 600 wa shule za sekondari na wasimamizi 604 ngazi ya mkoa na halmashauri ili kuboresha ufundishaji, ujifunzaji, usimamizi na uendeshaji wa shule kwa kutumia Teknolojia ya TEHAMA; na

v. Kusambaza vifaa vya TEHAMA katika shule 600 za msingi na 422 za sekondari ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia teknolojia ya TEHAMA.

#### 3.2.2. Mafunzo ya Amali katika shule za Sekondari na Vyuo vya Amali

i. Kukamilisha ujenzi wa majengo matatu (3) ya Kituo cha Umahiri katika Uendeshaji wa Usafiri wa Anga kilichopo Jijini Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi 12,749,439,852. Kituo hicho kitaimarisha ujifunzaji kwa wananfunzi wanaosoma masuala ya anga;

ii. Kuendelea na ujenzi wa vyuo vya VETA 64 za wilaya ambao umefikia wastani wa asilimia 67 na kimoja cha Mkoa wa Songwe kilichofikia asilimia 68;

iii. Kufungamanisha mifumo ya teknolojia ya elimu, kwa kuunganisha Mfumo wa Usimamizi wa Kujifunza (LMS) wa elimu ya sekondari, TET- Soma Kwanza TV, pamoja na madarasa janja yaliyopo Dar es Salaam, Pwani, Zanzibar (Shule ya Msingi Mtakuja) na Dodoma (Shule ya Sekondari Dr, Samia Suluhu Hassan) kwa lengo la kuongeza matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji;

iv. Kuandaliwa kwa Mpango wa pamoja kati ya waajiri, Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo Vikuu unaolenga kuwajengea uwezo wa ubunifu na ujasiriamali wanafunzi ili kuwawezesha kujiajiri au kuanzisha miradi binafsi;

v. Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya madarasa, kumbi za mihadhara, karakana katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) Kampasi ya Kikuletwa kwa gharama ya shilingi 21,481,716,931.61. Vilevile, ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme (*Hydropower Plant*) katika chuo hicho umefikia asilimia 60;

#### 3.2.3. Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu

i. Kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 348.77 kwa wanafunzi 107,541 wa mwaka wa kwanza ambapo kati yao wanafunzi wa shahada ya kwanza ni 94,451, wanafunzi wa shahada za juu ni 310 na wanafunzi wa diploma ni 11,844. Vilevile, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 550.44 imetolewa kwa wanafunzi 177,492

wanaoendelea na masomo ambapo kati yao wanafunzi wa shahada ya kwanza ni 170,413 wanafunzi wa Shahada za juu ni 108 na wanafunzi wa diploma ni 6,053;

ii. Kutoa ufadhili wa shilingi bilioni 10.5 kupitia ***SAMIA Scholarship*** kwa wanafunzi 1,786 wanaosoma masomo ya sayansi katika vyuo bora duniani;

iii. Kutoa ufadhili wa shilingi bilioni 5.487 kupitia **SAMIA *Extended DS/AI+*** wa kusoma Shahada ya Kwanza kwa wanafunzi 50 wenye ufaulu wa juu wa kidato cha sita katika fani za sayansi (PCM, PGM na PMC) waliochaguliwa kusoma fani za Sayansi Data, Akili Unde na Sayansi Shirikishi;

iv. Kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika kampasi za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Taasisi ya Sayansi za Bahari– Mjini Magharibi Zanzibar na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya – Rukwa;

v. Kuandaa mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za watanzania wanaoenda kusoma vyuo vya nje ya nchi kupitia Wakala waliosajiliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU); na

vi. Kukamilisha Mkakati wa Usawa wa Kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu wa Mwaka 2025/26- 2029/30 wenye lengo la kuimarisha mifumo na miundombinu itakayowezesha ufikiaji wa usawa wa kijinsia na Elimu Jumuishi katika Taasisi za Elimu ya Juu.

#### 3.2.4. Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

i. Kutoa mikopo ya shilingi milioni 667 katika awamu ya kwanza kwa wabunifu saba (07) kupitia Mfuko wa "*Samia Commercialization Fund*" ili kuwezesha ubiasharishaji wa bunifu na teknolojia zao. Miongoni mwa bunifu zilizokopeshwa ni pamoja na uchakataji na usambazaji wa asali bora na mafuta ya mawese kwa ajili ya masoko ya nje pamoja na mfumo wa kudhibiti foleni katika hospitali; na

ii. Kukamilisha na kuidhinisha Mkakati wa Kitaifa wa Kuhamasisha mchango wa Diaspora katika shughuli za Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

### 3.3. MAJI

Serikali imeendelea kutekeleza program na miradi ya maji ili kuongeza hali ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa kaya za wananchi wa mijini na vijijini kwa asilimia isiyopupungua 90. Katika kufikia azma hiyo, mikakati mbalimbali imeendelea kutekelezwa na kupata mafanikio yafuatayo:

i. Kukamilika kwa miradi 16 iliyotekelezwa katika Mikoa ya Dodoma, Njombe, Iringa, Kilimanjaro, Geita, na Tanga kwa gharama ya shilingi bilioni 16.28 na kunufaisha zaidi ya wananchi 118,400;

ii. Kuendelea na ujenzi wa miradi ya maji 71 inayotekelezwa maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mtwara, Tanga, Dodoma, Tabora na Dar es Salaam kwa gharama ya Shilingi bilioni 142.8 ambayo itanufaisha zaidi ya wananchi 2,887,029;

iii. Kulipa shilingi bilioni 198.84 kwa wakandarasi na wataalamu washauri wa miradi mbalimbali ikiwemo wa bwawa la Kidunda;

iv. Kulipa fidia ya shilingi bilioni 4.8 kwa wananchi 210 (Morogoro, Babati, Makambako na Tanga) ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maji.

v. Kusainiwa kwa mikataba mbalimbali ya utekelezaji wa miradi ya maji ambayo ni:

   a) Mkataba wa mradi wa kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira Morogoro utakaonufaisha zaidi ya wananchi 602,000 kwa gharama ya shilingi bilioni 81.4;

   b) Mkataba wa mradi wa usafishaji majitaka katika Jiji la Mwanza wenye thamani ya shilingi bilioni 38.7 na utakaonufaisha kaya 3,400;

   c) Mkataba wa miradi mitano wenye gharama ya shilingi bilioni 2.66 itakayotekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Geita, Singida na kunufaisha zaidi ya wananchi 186,580.

vi. Kukamilisha ununuzi na ufungaji wa Dira za Maji 2,271 za malipo ya kabla;

vii. Kuendelea na ujenzi wa mabwawa matatu (3) ya kuvuna maji ya mvua ya ukubwa wa kati katika maeneo ya Gidahababieg (Wilaya ya Hanang), Mwambazi (Wilaya ya Sumbawanga) na Mwamashindike (Wilaya ya Maswa) yenye ujazo wa mita za ujazo 1,457,000 ambayo yatanufaisha wananchi zaidi ya 1,817,800 na mifugo zaidi ya 356,400; na

viii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya dhana ya Mtandao wa Taifa wa Kusambaza Maji (National Water Grid) kwa kuanza utekelezaji wa miradi ifuatayo:

   a) Kukamilisha usanifu wa mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Dodoma kupitia Singida (Lake Victoria Dodoma Water Project - LVD);

   b) Kupata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya kutoa maji ziwa Tanganyika kuyapeleka kwenye Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa; na

   c) Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya kupeleka maji ya Mto Rufiji katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Lindi na maji ya Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara - Mikindani.

## SURA YA NNE

# 4. SEKTA ZA UZALISHAJI

## 4.1. KILIMO

Sekta ya Kilimo nchini ni muhimu katika usalama wa nchi, ujenzi wa uchumi na kukuza kipato cha wananchi. Kutokana na umuhimu huo Serikali imeendelea kuboresha sekta hii kupitia mipango mbalimbali ikiwemo; kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, kusambaza pembejeo za kilimo, kutoa mikopo kwa wakulima na kuongeza matumizi ya teknolojia ili kuwa na kilimo chenye tija na endelevu. Mafanikio makubwa yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kusambaza mbolea ya ruzuku tani 319,632 yenye thamani ya shilingi 512,465,277,981 kwa wakulima 532,023 na taasisi 777 katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kati ya gharama hizo, shilingi 384,223,259,670 ni mchango wa wakulima na shilingi 128,242,018,312 ni ruzuku ya Serikali;

ii. Kusambaza viuatilifu vya *sulphur* ya unga tani 44,177.18 na ya maji lita 2,142,874.50 yenye thamani ya shilingi 218,781,054,320 kwa wakulima wa korosho kwa mpango wa ruzuku katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Tanga, Pwani;

iii. Kuzalisha na kusambaza tani 37,557.18 za mbegu bora kwa mfumo wa ruzuku kwa wakulima wa mazao ya mahindi, alizeti na korosho. Kati ya tani hizo, tani 30,557.18 ni mbegu za mahindi na tani 7,000 ni mbegu za Alizeti. Vilevile, mbegu za korosho kilo 22,000 na viriba 13,000 vimesambazwa kwa wakulima wa korosho 30,000. Aidha, miche 21,740,920 ya kahawa imesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku;

iv. Kusajili na kurasimisha wakulima 532,023 (wanaume 360,318 na wanawake 171,705) kwenye mfumo rasmi wa mbolea ya ruzuku;

v. Kununua na kusambaza unit 200 za pampu, jenereta na mipira kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima 2,294 waliopo katika Mikoa ya Mara (368), Mwanza (398), Kagera (634), Ruvuma (383), Simiyu (74), Geita (292) na Tanga (145);

vi. Kutoa elimu ya matumizi ya mbegu bora, viuatilifu na mbolea kwa wakulima 442 (wanaume 326 na wanawake 116) na vijana 141 kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) wakati wa maonesho ya mbegu yaliyofanyika katika Mikoa ya Singida na Dodoma.

vii. Kuanzisha mashamba darasa 329 na mashamba ya mfano 185 kwa mazao ya alizeti, mahindi na mazao jamii ya mikunde katika mikoa 10, Halmashauri 39 na kata 195 zinazotekeleza Programu ya AFDP yaliyonufaisha wakulima 6,492 (wanaume 3,455 na wanawake 3037);

viii. Kuongezeka kwa uzalishaji wa chai kavu kutoka kilo 4,251,010 Septemba 2025 hadi kufikia kilo 9,354,345 Desemba, 2025, sawa na ongezeko la asilimia 44;

ix. Kufungua viwanda vipya vya kuchakata chai katika Wilaya ya Njombe (Mlangali Tea Factory); Bukoba (Maruku Tea Factory), Wanging'ombe (Kibena Tea Factory), Njombe (Ikanga Tea Factory), Ludewa (Luponde Tea Factory), na Mufindi (Itona Tea Factory); na

x. Kuongezeka kwa mauzo ya mnada wa chai wa Dar es Salaam kutoka kilo 127,000 Oktoba, 2025 hadi kilo 346,780 Januari, 2026 pamoja na wastani wa bei kwa kilo moja ya chai kavu mnadani kutoka Dola ya Marekani 1.1 Oktoba, 2025 hadi 1.6 Januari, 2026.

### 4.2. MIFUGO NA UVUVI

Mifugo na Uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi, uzalishaji wa ajira na kuongeza kipato kwa wananchi. Katika kuimarisha sekta hiyo, Serikali imeendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya shughuli za ufugaji na uvuvi ikiwemo ujenzi wa majosho na vizimba vya kufugia Samaki. Jitihada hizo zimewesha kupatikana kwa mafanikio yafuatayo:

i. Kutoa chanjo kwa mifugo 2,239,755 katika kipindi cha Novemba, 2025 hadi Januari, 2026 ili kukinga mifugo dhidi ya magojwa mbalimbali;

ii. Kujenga mabwawa 15 katika vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbemaji vilivyopo Mikoa ya Morogoro (Kingolwira - 10) na Igunga Tabora (Mwamapuli - 5) ili kuongeza uzalishaji wa vifaranga na utoaji huduma za ugani;

iii. Kuanza ujenzi wa soko la Samaki, (Kipumbwi) katika Mkoa wa Tanga kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.3 ambapo ujenzi umefikia asilimia 15. Kukamilika kwa soko hilo, kutanufaisha wananchi kupitia ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja 10,000;

iv. Kuendelea kwa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Kilwa masoko ambapo hadi Januari 2026, ujenzi umefikia asilimia 92 na unatarajiwa kukamilika Machi 2026. Kukamilika kwa mradi huo kutazalisha ajira takriban 30,000;

v. Kufunguliwa kwa dirisha la maombi kwa wananchi, vikundi vya wavuvi na vyama vya ushirika kwa ajili ya kukopeshwa boti 100 zitakazonufaisha wavuvi wa maeneo mbalimbali nchini; na
vi. Kutolewa kwa shilingi bilioni 7.0 kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa vijana 308 wanaofuga samaki kwa vizimba.

### 4.3. VIWANDA NA BIASHARA

Serikali imeendelea kuweka jitihada katika kujenga uchumi wa viwanda wenye ushindani unaolenga kuzalisha ajira hasa kwa vijana na wanawake, huku ikikuza uchumi wa nchi na kipato cha mwananchi mmoja mmoja. Jitihada hizi zinalenga kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha viwanda na biashara katika ngazi ya kikanda na kimataifa. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kutoa mikopo 193 yenye thamani ya shilingi milioni 1,085,900,000 kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi na Mfuko wa Kudhamini Mikopo kwa Wajasiriamali katika mikoa 19 ya Tanga, Tabora, Katavi, Pwani, Rukwa, Iringa, Morogoro, Ruvuma, Mwanza, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Songwe, Shinyanga, Dodoma, Singida, Manyara, Kagera na Kigoma. Mikopo hiyo imezalisha ajira 265. Aidha, mafunzo ya ujasiriamali yametolewa kwa vijana 1,200 na kusajili vijana 278 kwenye programu za uatamizi wa biashara;
ii. Kurasimisha biashara mbalimbali kwa kusajili kampuni 4,233, majina ya biashara 7,498, kutoa leseni za viwanda 141 na kusajili alama za biashara na huduma 881 ili kuwalinda wabunifu. Urasimishaji huo umeongeza ajira na kuendelea kuchagiza uchumi wa nchi;
iii. Kufanya mafunzo kwa wajasiriamali wadogo katika mikoa 15 ya Dodoma, Iringa, Mwanza, Simiyu, Mara, Ruvuma, Arusha, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Geita, Pwani, Kagera, Kilimanjaro na Mtwara ambapo jumla ya Wajasiriamali 1,059 walipatiwa mafunzo;
iv. Kukamilisha tathmini ya awali katika kongani na mitaa ya viwanda katika Mikoa 11 ya Manyara, Singida, Mbeya, Iringa, Shinyanga, Ruvuma, Morogoro, Kilimanjaro, Dodoma, Tabora na Kigoma;
v. Kuzalisha lita 83,333 za dawa ya Viuadudu zenye thamani ya shilingi 1,03,922,243.84 na lita 6223 za Viuatilifu aina ya Thurisave-24 (T-24) zenye thamani ya shilingi 62,230,000.00 kupitia kiwanda cha Tanzania Biotech Products Limited ambapo lita 600 za dawa ya Viuadudu zenye thamani ya shilingi 89,079,284.00 na Viuatilifu lita

6,223 zenye thamani ya shilingi 62,239,000.00 zimeuzwa. Aidha, kiwanda hicho kimezalisha jumla ya lita 792 za mbolea hai aina ya Fosforina kwa ajili ya kufanyiwa majaribio na TFRA na TARI katika kipindi cha msimu wa kilimo cha Februari 2026;

vi. Kuanza kwa tafiti ya Madini Adimu na ya Kimkakati (Critical Minerals) kupitia Taasisi ya TIRDO katika Wilaya ya Kyerwa Mkoa wa Kagera na Ikungi Mkoa wa Singida. Matokeo ya utafiti huo yatavutia uwekezaji mkubwa utakaoleta manufaa makubwa kwa nchi;

vii. Kuainishwa kwa maeneo matatu (03) ya kongani za viwanda katika Mikoa ya Mbeya, Singida na Kigoma na mtaa mmoja (01) wa viwanda katika Mkoa wa Morogoro; na

viii. Kuanzisha programu maalum ijulikanayo kama SAMIA UBORA KLINIKI, yenye lengo la kuwezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kuzalisha bidhaa bora na salama kwa kuzingatia matakwa ya viwango na uthibitishaji ubora kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Kupitia programu hiyo:

   a) Wajasiriamali wadogo na wa kati 1,059 (akiwemo vijana 371) katika mikoa 15 wamepata mafunzo bila malipo kupitia SIDO kuhusu uzalishaji wa bidhaa bora na salama, uongezaji thamani, usimamizi wa biashara na masoko;

   b) Sampuli 800 za bidhaa za wajasiriamali zimepimwa bure kwenye maabara za TBS ili kuhakiki ubora na usalama wa bidhaa kabla ya kuingia sokoni na kurasimisha zilizopo sokoni kwa kuzipatia alama ya ubora; na

   c) Bidhaa 192 za wajasiriamali zimepata leseni na vyeti vya kutumia alama ya ubora ya TBS bila kulipia gharama za ukaguzi na upimaji. Hatua hii imewezesha bidhaa kuingia katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa; na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa, kipato cha kaya na fursa za ajira.

## 4.4. MADINI

Sekta ya madini ni miongoni mwa sekta muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa kutokana na mchango wake katika kuimarisha mapato ya Serikali na kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kuandaa na kusimamia sera, mikakati na mipango mbalimbali ya kuendeleza sekta ya madini. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kukusanya mapato ya madini shilingi bilioni 311.80 ikiwa ni sawa na asilimia 111 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 280.64 kwa kipindi cha Novemba 2025 hadi tarehe 25 Januari, 2026;

ii. Kukamilisha Mkakati wa Uongezaji Thamani ya Madini wa miaka mitano (5) kuanzia 2026/2027 hadi 2030/2031;

iii. Kuongeza akiba ya dhahabu kwa kununua jumla ya tani 17.03 zenye thamani ya Shilingi Trioni 4.97;

iv. Kusimamia uuzwaji wa tani 14.66 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 3.75 katika viwanda vya usafishaji dhahabu nchini;

v. Kuchambua sampuli 19,705 za kijiolojia katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kufanya utafiti wa madini (Quarter Degree Sheet - QDS) 221 na 222 yaliyopo katika Wilaya za Kibiti na Rufiji, na kuongeza eneo lililofanyiwa utafiti wa jiolojia kufikia asilimia 98;

vi. Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Jemolojia Tanzania Jijini Arusha chenye thamani ya shilingi bilioni 33 ambapo ujenzi umefikia asilimia 10;

vii. Kusimika mitambo ya uzalishaji wa Nishati ya Rafiki (Briquettes) katika Mikoa ya Tabora na Dodoma. Aidha, makontena ya kuhifadhia na kuuzia mkaa safi yamesambazwa katika Mikoa ya Njombe, Mbeya, Songwe, Pwani, Dodoma, Iringa, Ruvuma, Geita na Shinyanga;

viii. Kuendelea na usimikaji wa mtambo wa kusafisha chumvi uliopo eneo la Llingaula Wilayani Kilwa Mkoani Lindi ikiwa ni njia ya kuongeza thamani madini ya chumvi;

ix. Kuendelea na upanuzi wa mitambo ya uchenjuaji iliyopo Lwamgasa na Katente Mkoani Geita na Itumbi Mkoani Mbeya;

x. Kuboresha mfumo wa kielektroniki unaoratibu masoko ya madini kwa kuunganisha mfumo huo na mfumo wa usimamizi na utoaji wa leseni pamoja na kuunganisha na mashine ya kupima ubora wa madini;

xi. Kuanza ujenzi wa Maabara kubwa ya Kisasa (State of Art Geo-scientific Laboratory) ya uchunguzi wa sampuli za madini katika eneo la Kizota Mkoani Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni 14.3 ambao umefikia asilimia 11.5 pamoja na ujenzi wa maabara katika Mkoa wa Geita na Wilaya ya Chunya ambao umefikia wastani wa asilimia 6; na

xii. Kukamilisha usimikaji wa vituo 32 vya kufuatilia mwenendo wa mitetemo ya ardhi pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya utafiti wa jiofizikia na matetemeko ya ardhi.

### 4.5. MALIASILI NA UTALII

Sekta ya Maliasili na Utalii inaendelea kuwa sekta muhimu nchini katika kuchangia Pato la Taifa (GDP), ajira na fedha za kigeni. Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuimarisha uhifadhi, masoko na ujenzi wa miundombinu ya kukuza utalii, na

kuongeza mchango wa utalii katika maendeleo ya Taifa. Mikakati hiyo imewezesha kupatikana kwa mafanikio yafuatayo:

i. Kuandaa mkakati mpya wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano baina ya Binadamu na Wanyamapori wa miaka kumi (2025/26 – 2035/36) ili kulinda usalama wa wananchi na mali zao;
ii. Kukamilisha taarifa ya Matokeo ya Sensa ya Kitaifa ya Wanyamapori Nchini ambayo imefanyika kwa mara ya kwanza nchi nzima baada ya miaka 10;
iii. Kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa barabara ya tabaka gumu yenye urefu wa kilomita 88 kuanzia lango kuu la Loduare katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro hadi Golini, mpakani mwa hifadhi ya Taifa Serengeti ambapo mkandarasi amekabidhiwa saiti;
iv. Kukamilisha ujenzi wa mfumo wa kidigiti wa *AI Chatbot* ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa za vivutio vya utalii na kuwezesha watalii kupata taarifa za kina kuhusu vivutio vya utalii nchini;
v. Kuandaa Mkakati wa Maendeleo Endelevu ya Utalii katika Ukanda wa Pwani na Baharini (2025 – 2035) unaolenga kukuza utalii wa fukwe na utamaduni katika Ukanda wa Pwani kuanzia fukwe za Moa - Tanga hadi Msimbati – Mtwara;
vi. Kutoa tuzo za ushindani kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Utalii na Uhifadhi zijulikanazo kama "*Serengeti Awards*" kwa lengo la kuwatambua na kuthamini mchango wao katika kuhamasisha ubunifu, kukuza utalii endelevu na kuitangaza nchi kimataifa ili kuimarisha taswira ya Tanzania kama nchi yenye vivutio bora vya utalii Duniani.

## 4.6. ARDHI

Sekta ya ardhi ni rasilimali muhimu kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uzalishaji ikiwemo kilimo, viwanda, uchimbaji wa madini na maendeleo ya makazi. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kuhimiza matumizi ya TEHAMA na mikakati ya kuongeza uwazi na ufanisi katika utoaji huduma za ardhi. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

### 4.6.1. Usimamizi wa Ardhi

i. Kumilikisha ardhi kwa wananchi na kusajili hatimiliki 22,501, hatimiliki za kimila 31,459, hatimiliki za sehemu ya jengo (unit tittles) 169 na nyaraka nyingine za kisheria 19,248;
ii. Kutatua migogoro 5,860 ya kiutawala ambapo migogoro 2,116 imetatuliwa kupitia njia ya kawaida na migogoro 3,744 imetatuliwa kupitia kliniki za Ardhi;

iii. Kuidhinisha maombi 116 ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta 1,090.75. Kati ya maombi hayo, maombi 32 ni ya raia wa Tanzania wanaomiliki ukubwa wa hekta 25.69 na hekta 84 ni ya wawekezaji kutoka nje ya nchi wanaomiliki ukubwa wa hekta 1,065.06. Uwekezaji kutoka nje ya nchi una mtaji wenye thamani ya dola za Marekani milioni 222.35;

iv. Kuongeza alama mpya za upimaji kumi na tatu (13) katika maeneo mbalimbali nchini;

v. Kukamilisha uhakiki na uandaaji wa ramani ya mpaka wa kimataifa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kenya katika kipande cha awamu ya kwan-za ya uimarisha mpaka yenye kilomita 238 (Ziwa Viktoria hadi Ziwa Natron);

vi. Kujenga uwezo na kusajili wananchi 15,979 kwa ajili ya kutumia mfumo wa e-Ardhi kupata huduma za ardhi mahali popote;

vii. Kuimarisha huduma za uthamini kupitia mfumo ambapo kuanzia tarehe 1 Novemba 2025 hadi 15 Januari, 2026 ripoti za uthamini 7,550 zilijisajiliwa kwenye mfumo huo;

viii. Kuratibu uthamini wa mali za wananchi 1,800 kwa ajili ya malipo ya fidia katika Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) awamu ya Sita kipande cha kutoka Tabora hadi Kigoma Kilomita 414; na

ix. Kuratibu uthamini wa mikuza ya utafiti (Source Lines) yenye urefu wa kilomita 2,047.9 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi 2,571 wenye mali zenye thamani ya shilingi 477,903,523.33 katika vijiji 27 vya Mkoa wa Lindi na Mtwara wanaopisha mradi wa utafiti wa mafuta na gesi katika kitalu cha Lindi - Mtwara.

### 4.6.2. Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi

i. Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na kufanya uhakiki na upimaji wa vijiji 40 katika Halmashauri za Wilaya tano (5) ambazo ni Masasi (8), Kisarawe (8), Misungwi (8), Muheza (8), Mbeya (8) katika Mikoa (5) ya Mtwara, Pwani, Mbeya, Tanga na Mwanza;

ii. Kuandaa mipango kina 13 katika Wilaya 3 za Sikonge, Nyang'hwale na Ukerewe katika maeneo ya mashamba na makazi;

iii. Kuandaa na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila 1,985 kupitia mfumo wa *National Land Use Information System* (NLUIS) katika Halmashauri za Wilaya 3 ambazo ni Sikonge (576), Ukerewe (773) na Nyanghwale (606); na

iv. Kutatua migororo ya ardhi ya vijiji 22 katika Wilaya za Masasi vijiji (6), Kisarawe (4), Muheza (8), Mbeya (2) na Misungwi (2).

#### 4.6.3. Mipango Miji na Vijiji

i. Kuandaa mipango ya uendelezaji na utangazaji wa maeneo mapya yaliyoiva kimipangomiji ambapo, jumla ya maeneo 29 ya upangaji yaliyoiva kimipangomiji yameidhinishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Aidha jumla ya michoro ya mipangomiji 168 yenye jumla ya viwanja 24,787 vya matumizi mbalimbali imeidhinishwa; na

ii. Kutambua na kurasimisha makazi 30,843 na hivyo kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya miundombinu na huduma za kijamii katika maeneo hayo.

### 4.7. NISHATI

Serikali imeendelea kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji endelevu wa nishati kwa kutekeleza miradi na kuboresha miundombinu ya usafirishaji wa nishati. Jitihada hizo zimewezesha nchi kuwa na nishati ya uhakika na kuchagiza maendeleo ya sekta nyingine. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

i. Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kupeleka Umeme katika vitongoji 9,009 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.2 ambapo hadi kufikia Januari, 2026 jumla ya vitongoji 39,888 kati ya 64,359 vimeunganishwa na umeme, sawa na asilimia 62;

ii. Kukamilisha Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa mradi wa kuzalishaji umeme wa Megawati 50 kwa kutumia jua unaotekelezwa katika Wilaya ya Kishapu, Mkoa wa Shinyanga. Hatua inayofuata ni kufanya majaribio (*testing*), ili uingizwe katika Gridi ya Taifa;

iii. Kutekeleza miradi 235 ya kusambaza umeme kwa wateja kupitia Mpango Mahsusi wa Nishati ambayo imewezesha kuunganishiwa umeme wateja wapya 134,811; na

iv. Kuendelea kutekeleza mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini ambao unalenga kuokoa mazingira, afya za watumiaji na muda uliokuwa unapotea wakati wa utafutaji wa kuni pamoja na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Jitihada hizo zimewezesha yafuatayo:

   a) Taasisi 89 zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku zimehamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa, hivyo kufikia jumla ya taasisi 1,136 zinazotumia nishati safi ya kupikia hadi sasa;

   b) Kaya 470 na shule moja katika Mkoa wa Lindi, na Kaya 530 katika Mkoa wa Pwani zimeunganishwa na gesi asilia kwa ajili ya kupikia;

   c) Majiko banifu 13,575 yenye ruzuku ya asilimia 85 na Mitungi ya LPG 28,653 ya kilo sita (6) yenye ruzuku ya asilimia 50 imegawiwa kwa wananchi.

**SURA YA TANO**

# 5. UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

## 5.1. UJENZI

Serikali imeendelea kujenga miundombinu wezeshi ya usafiri na usafirishaji wa watu na bidhaa ili kuimarisha mtiririko wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha siku 100 za Serikali ya Awamu ya Sita, miradi mbalimbali ya sekta ya ujenzi imetekelezwa ikiwemo:

i. Kukamilisha ujenzi wa miradi 40 ya madaraja ya dharura kupitia programu maalumu ya *Contigent Emergency Response Component* (CERC) kwa gharama ya shilingi bilioni 291.1;

ii. Kukamilisha ujenzi wa barabara ya "*Three (3) Connecting Roads to Industrial Park at Old Airport*" yenye urefu wa kilomita 1.5 kwa kiwango cha Lami katika Mkoa wa Mbeya;

iii. Kusaini mkataba wa ujenzi wa barabara ya Makambako – Songea sehemu ya Rutukila – Songea yenye urefu wa kilomita 95.1 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 158.67;

iv. Kuwezesha malipo ya shilingi bilioni 105.876 kwa wakandarasi 133 waliojenga barabara na madaraja;

v. Kuendelea na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambapo ujenzi wa miundombinu umekamilika na ujenzi wa majengo umefikia asilimia 67.94;

vi. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kupunguza msongamano katika miji na majiji ambapo utekelezaji kwa baadhi ya miradi ni kama ifuatavyo:

   a. BRT Awamu ya 3: Mradi huu unahusisha barabara ya Nyerere kuanzia makutano ya barabara ya Kivukoni na Mtaa wa Azikiwe hadi Gongolamboto (km 23.33) ambapo ujenzi umefikia asilimia 98;

   b. BRT Awamu ya 4: Mradi huu unahusisha barabara ya Ali Hassan Mwinyi – Morocco – Mwenge – Tegeta; Mwenge – Ubungo (km 30.12) ambapo ujenzi umefikia asilimia 45;

   c. Upanuzi wa barabara ya Uyole – Ifisi - Songwe Airport Jijini Mbeya yenye urefu wa kilometa 29 kutoka njia 2 kuwa njia 4 utekelezaji umefikia asilimia 41;

   d. Ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya mzunguko katika Jiji la Dodoma unaohusisha ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mzunguko wa nje yenye jumla ya urefu wa kilometa 112.3 (Ihumwa Dry Port – Matumbulu –

Nala: km 60) ujenzi umefikia asilimia 94; na (Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port: km 52.3) ujenzi umefikia asilimia 91; na

e. Ujenzi wa barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3) ujenzi umefikia asilimia 28.

vii. Kuendelea na ukarabati mkubwa wa Vivuko vya MV Magogoni na MV Kigamboni kwa gharama ya shilingi bilioni 10.278 ambapo ukarabati umefikia asilimia 81.3 na 30 mtawalia.

## 5.2. UCHUKUZI

Sekta ya Uchukuzi ni kichocheo muhimu katika maendeleo ya kiuchumi kwa kurahisisha usafiri na usafirishaji wa watu, bidhaa na huduma, hivyo kurahisisha utekelezaji wa shughuli za biashara ndani na nje ya nchi. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya sekta ya uchukuzi ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa, viwanja vya ndege na uboreshaji wa bandari ili kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za usafirishaji. Katika kipindi cha siku 100, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kukamilika na kuzinduliwa kwa Meli ya New MV Mwanza tarehe 23 Januari, 2026 yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo, magari madogo 20 na magari makubwa 3 kwa wakati mmoja. Meli hiyo imeongeza upatikanaji wa uhakika wa huduma za usafiri katika Ziwa Victoria na kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii;

ii. Kuendelea na maboresho ya Reli ya TAZARA ambapo mkataba wa ufufuaji na uboreshaji wa reli hiyo ulisainiwa tarehe 29 Septemba, 2025 na kuzinduliwa tarehe 20 Novemba, 2025 nchini Zambia. Kukamilika kwa reli hiyo, kutasaidia kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam, kuimarisha usafiri kati ya Tanzania na nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na kuchochea fursa za kiuchumi katika maeneo na mikoa ambayo reli hiyo inapita na Taifa kwa ujumla;

iii. Kuendelea na ujenzi wa matenki 15 ya mafuta katika bandari ya Dar es Salaam ambao umefikia asilimia 25 na magati mawili (2) kati ya 10 ambao umefikia asilimia 5. Ujenzi huo utawezesha bandari hiyo kuhudumia tani milioni 60 za shehena kwa mwaka na hivyo kuongeza urahisi wa biashara na usafirishaji kwa wafanyabiashara na watanzania kwa ujumla;

iv. Kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la Viongozi (*Presidential Pavillion*) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere – (Terminal I) lenye uwezo wa

kuhudumia wakuu wa nchi watano (5) kwa wakati mmoja na hivyo kupunguza msongamano katika majengo mengine ya abiria;

v. Kukamilika kwa ujenzi wa Bandari ya Kemondo na Bukoba katika Ziwa Victoria ambazo ni vituo vya usafirishaji katika maeneo ya Bukoba, Mwanza na Bandari za Uganda na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii; na

vi. Kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji cha Kikanda – (*Maritime Rescue Cordination Centre* – MRCC) katika Ziwa Victoria ambacho kitaimarisha usalama wa watu, mizigo na vyombo vya usafiri.

### 5.3. MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari nchini kwa lengo la kuongeza chachu ya matumizi ya teknolojia katika shughuli za kiuchumi, kijamii, kisiasa na usalama kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia ulimwenguni. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo;

i. Kukamilika kwa ujenzi wa minara 758 katika kata 713 kwa gharama ya shilingi bilioni 126 ambapo jumla ya wananchi milioni 8.5 wamenufaika na huduma za mawasiliano ya simu na intaneti. Vilevile, ujenzi wa minara 636 Vijijini (621 simu na 15 Redio) umefikia asilimia 78 ikiwa ni ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na asilimia 55 Oktoba, 2025. Kukamilika kwa ujenzi wa Minara ya Mawasiliano kunawezesha Wananchi kupata huduma za kifedha kwa njia ya simu, biashara mtandaoni, elimu na afya; huduma za simu na intaneti; kuimarisha ushiriki wa wananchi wa vijijini katika shughuli za kiuchumi; na kupunguza pengo la kidijitali kati ya vijijini na mijini;

ii. Kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa minara ya simu 201 katika kata 201 zenye vijiji 263 tarehe 5 Disemba, 2025 utakaogharimu shilingi bilioni 19.8. Mradi huu unatarajiwa kunufaisha wananchi takribani milioni 2.8;

iii. Kuunganishwa kwa wilaya 10 (Kilwa, Maswa, Bariadi, Sikonge, Urambo, Ushirombo, Chunya, Karagwe, Nzega, na Butiama) kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufanya jumla ya wilaya 119 kati ya 139 zilizounganishwa;

iv. Kufunga vifaa vya mikutano ya video (Video Conferencing) kwenye vituo 100. Vituo vilivyounganishwa na huduma hiyo ni taasisi za Haki Jinai ambazo ni Ofisi za Taifa za Mashitaka (20); Magereza (38); Jeshi la Polisi Tanzania Bara (34); na Jeshi la Polisi Zanzibar (6) pamoja na Ofisi za Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari – Mtumba (2);

v. Kufanya uhakiki wa Anwani 48,492 katika Halmashauri tatu (3) za Jiji la Mbeya, Songea na Manispaa ya Iringa. Katika uhakiki huo jumla ya Anwani mpya 8,094 ziliweza kusajiliwa na kufanya Anwani zilizokusanywa kuongezeka kutoka Anwani 238,958 zilizokuwepo awali hadi 247,052 sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Uhakiki wa Anwani za Makazi utapelekea yafuatayo: Kuimarika kwa Upatikanaji wa Huduma za Jamii; Kukuza Biashara, Uchumi wa Kidijitali na Ajira; Kuimarisha Huduma za Posta na Usafirishaji wa Mizigo; na Kuimarisha Usalama na Mipango ya Miji na Vijiji;

vi. Kufikisha huduma ya Wi-Fi katika maeneo ya Umma 61 kati ya 120 sawa na asilimia 51 ya lengo. Hatua hii, inalenga kuchochea matumizi ya intaneti nchini;

vii. Kukamilika kwa ujenzi wa mfumo wa *Jamii Portal* ambao utatumika kutoa huduma kwa wananchi kupitia vituo 32 vya huduma;

viii. Kuunganisha taasisi 800 za umma kwenye Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (GovNet); na

ix. Kukamilika kwa ujenzi wa Mfumo wa Tembo Portal, utakaotumiwa na wananchi kuweka miadi (appointments) ya kukutana na viongozi wa Wizara (Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu) kwa lengo la kuwasilisha kero na changamoto zinazowakabili katika Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA.

## SURA YA SITA

## 6. ULINZI NA USALAMA

Serikali imeendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hususan maeneo ya kimkakati kama vile bandari, viwanja vya ndege, na mipakani ili kudumisha amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao. Jitihada mbalimbali zimechukuliwa ili kuimarisha ulinzi na usalama ikiwemo kufunga vifaa vya kisasa vya ulinzi vya TEHAMA, kuwezeshwa vifaa, zana za kisasa, mafunzo na mazoezi. Kutokana na jitihada hizo, mafanikio yafuatayo yamepatikana:

i. Kuendelea kuimarisha hali ya ulinzi na usalama nchini pamoja na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Kuendelea kuimarisha ulinzi wa maeneo muhimu ya kimkakati ikiwemo mradi wa kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere; Reli ya Kisasa (SGR); Mgodi wa Tanzanite uliopo Mirerani Mkoa wa Manyara; Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutokea nchini Uganda hadi Mkoani Tanga; Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia Likong'o Mkoa wa Lindi; Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara; na Viwanja vya Ndege;

iii. Kuendelea kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa na Kikanda katika operesheni za ulinzi wa amani ikiwemo ulinzi wa amani kwenye nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Lebanon chini ya Misheni za Umoja wa Mataifa. Vilevile, inashiriki katika mapambano dhidi ya ugaidi nchini Msumbiji kupitia makubaliano ya uwili (Bilateral agreement) kati ya Tanzania na Msumbiji;

iv. Kuendelea kutoa mafunzo kwa vijana 34,000 kuhusu maadili mema, uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na kuwapatia stadi za kazi katika nyanja mbalimbali;

v. Kupokea magari 51, boti tatu (3) na helikopta moja (1) kwa ajili ya kuzima moto na uokoaji;

vi. Kufanya ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto pamoja na majanga mengine katika maeneo 5,342 kote nchini; na

vii. Kutambua na kusajili watu 117,002 hivyo kufanya watu waliosajiliwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) mpaka sasa kufikia 26,442,997. Vilevile, Serikali imezalisha namba za utambulisho (NIN) 113,886 na hivyo kufikisha NIN 22,326,111 zilizozalishwa. Aidha, vitambulisho vya NIDA 1,028 vimezalishwa na hivyo kufanya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 21,340,123.

**SURA YA SABA**

## 7. UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Utumishi wa umma na Utawala bora ni nguzo muhimu katika kuhakikisha huduma za jamii zinatolewa kwa haki na usawa pamoja na kuimarisha utawala wa sheria nchini. Kwa kuzingatia hilo, Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya utumishi wa umma na utawala bora ili kujenga imani ya wananchi kwa taasisi za umma. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

### 7.1. UTUMISHI

i. Kuajiri wahudumu wa afya 5,000 na walimu 7,000 ambao wamepangiwa vituo vya kazi na kuongeza hali ya utoaji wa huduma za afya pamoja na kupunguza upungufu wa walimu wa sayansi katika maeneo mbalimbali nchini; na

ii. Kuboresha Mfumo wa e-Mrejesho utakaowezesha wananchi kutoa taarifa au malalamiko na kupata majibu kuhusu masuala waliyowasilisha. Aidha, maboresho yaliyofanyika yamewezesha kupanuka kwa wigo wa viongozi wanaotumia mfumo huo na kufanya kuwa rafiki kwa wananchi kuwasilisha hoja kwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji wengine.

### 7.2. UTAWALA BORA

i. Kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi 2,905 katika Mikoa ya Morogoro na Singida ambapo jumla ya migogoro 14 ilitatuliwa kati ya 186 iliyopokelewa. Aidha, migogoro 172 imekabidhiwa kwa Watendaji kwa ajili ya kutatuliwa;

ii. Kukamilisha Mwongozo wa Utendaji Kazi wa Mabaraza ya usimamizi wa utajiri asili na Maliasilia za nchi pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu uangalizi na usimamizi wa utajiri asili na maliasilia za nchi;

iii. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) vya Geita na Simiyu pamoja na mahakama za mwanzo 39; na

iv. Kushughulikia mashauri ya kesi za madai na usuluhishi ambapo Serikali imeshinda mashauri matatu (03) ya usuluhushi. Kati ya mashauri hayo, mashauri mawili (02) ni ya usuluhishi wa kitaifa na shauri moja (01) ni la usuluhishi wa kimataifa.

## SURA YA NANE

## 8. USHIRIKANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

Serikali imeendelea kulinda na kusafisha taswira ya Taifa letu katika nyanja ya kidiplomasia, pamoja na kushawishi jumuiya ya wanadiplomasia kuhusu kuendelea kushirikiana na Tanzania kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa. Kutokana na juhudi hizo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kufanikisha mashauriano ya kimkakati na Jumuiya ya wanadiplomasia ndani na nje ya nchi kwa lengo la kulinda na kushamirisha taswira ya Taifa letu kikanda na kimataifa;

ii. Kufikisha ujumbe maalum wa Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wenye maelezo na ufafanuzi wa kina kuhusu mazingira chanya ya kisiasa, kiuchumi na kijamii nchini katika nchi za kimkakati zilizopo Amerika, Ulaya na Mashariki ya Kati; na

iii. Kufanikisha mashauriano baina ya Serikali na wabia wa maendeleo nchini na katika nchi za kimkakati zilizopo Amerika, Ulaya na Mashariki ya Kati kwa lengo la kushawishi nchi rafiki na mashirika ya kikanda na kimataifa kuendelea kushirikiana na Tanzania kupitia Ushirikiano wa Uwili, Kikanda na Kimataifa.

## SURA YA TISA

## 9. KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO

Sekta ya Kazi, Ajira na Mahusiano imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa na kuboresha ustawi wa jamii kwa kuhakikisha uwepo wa mazingira bora ya kazi, ajira zenye staha na mahusiano mema kati ya waajiri na wafanyakazi. Kupitia utekelezaji wa sera, sheria na mikakati mbalimbali, mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

i. Kuunganisha jumla ya watanzania 2,002 na fursa za ajira nje ya nchi. Hatua hii itawezesha kuongeza kipato cha wananchi, kupunguza ukosefu wa ajira, kuongeza fedha za kigeni na kukuza ujuzi;

ii. Kuwezesha vijana 500 madereva pikipiki kupata fursa za ajira Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Fursa hizo zilitangazwa tarehe 29 Desemba, 2025 ambapo usaili unaendelea na watakaofaulu wanatarajiwa kuondoka Februari, 2026;

iii. Kuandaliwa kwa Mtaala wa Mafunzo kwa Watanzania wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi (*Pre-Departure Orientation Training Curriculum*). Mtaala huo utatumika kuwaandaa watanzania wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi ili kulinda usalama wao, ufanisi kazini, ustawi wa kiuchumi na kijamii;

iv. Kuandaliwa kwa Mwongozo wa Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Sekta isiyo Rasmi ili kuongeza wigo wa huduma za Hifadhi ya Jamii kwa wananchi waliojiajiri;

v. Kutangaza Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara kwa Sekta Binafsi Na.605A iliyoanza kutumika rasmi Januari, 2026, kwa lengo la kuboresha ustawi wa wafanyakazi;

vi. Kuzindua Kamati ya Majadiliano baina ya Serikali, Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri kwa lengo la kuwa na uelewa na mtazamo wa pamoja, kupunguza migogoro na migongano baina ya wadau na hatimaye kuongeza ufanisi na tija katika sekta ya kazi; na

vii. Kukamilisha Programu ya Nchi ya Kazi za Staha (*Decent Work Country Program*) inayolenga kukuza ajira zenye heshima na usalama kwa kuimarisha ujuzi wa wafanyakazi, haki za kazi, kinga ya jamii na majadiliano ya pamoja sehemu za kazi.

## SURA YA KUMI

## 10. URATIBU WA MASUALA MBALIMBALI

### 10.1. MAZINGIRA

Uhifadhi wa mazingira ni muhimu kwa ajili ya usalama wa chakula, upatikanaji wa maji, na kinga dhidi ya majanga ya asili kama ukame na mafuriko yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kulinda mazingira na kupunguza Athari za mabadiliko ya tabianchi. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hiyo ni kama ifuatavyo:

i) Taasisi 89 zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku zimehamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa, hivyo kufikia jumla ya taasisi 1,136 zinazotumia nishati safi ya kupikia hadi sasa;

ii) Kushiriki katika Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) uliowezesha nchi kupata ahadi za fedha za utekelezaji wa miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 870 na Euro 500,000. Fedha hizi ni kwa ajili ya miradi ya maji, kilimo, nishati, afya na biashara ya kaboni na uchumi wa buluu;

iii) Kuchaguliwa kwa Tanzania kuwa Kituo cha Kikanda cha kuratibu utoaji wa msaada wa kitaalam kwa nchi za Afrika zinazokabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi;

iv) Kusajili miradi 9 ya biashara ya kaboni na hivyo kufikia miradi 82 iliyosajiliwa hadi Januari 2026. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji;

v) Kuongezeka kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya Mazingira kupitia mifuko ya kimataifa ya Hifadhi ya Mazingira na mabadiliko ya Tabianchi ambapo shilingi bilioni 98.2 zimepatikana kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi ya kuhifadhi mazingira.

vi) Kupanda miti 705,300 katika vyanzo vya maji ili kuhifadhi uoto wenye kutunza vyanzo hivyo.

### 10.2. MAENDELEO YA JAMII

Serikali imeendelea kujenga msingi wa jamii bora yenye nidhamu, utu na ushiriki wa makundi yote katika shughuli za maendeleo ili kuwa na Taifa lenye ustawi wa jamii na maendeleo endelevu kwa makundi yote. Katika kutekeleza hayo, Serikali imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo:

i) Kutenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya mitaji ya kuwezesha biashara ndogo, za kati na uendeshaji wa Kampuni -changa (start – ups) ambazo zitatolewa kwa awamu kama ifuatavyo:

a. Awamu ya kwanza itahusisha utoaji wa shilingi 48,685,829,751.00 kwa wanufaika 15,483 ambao ni Wavuvi wadogo (4,561), wakulima (375), kampuni changa (50), wasanii (3,957), wajasiriamali wenye viwanda vidogo na vya kati (4,040) na wafanyabiashara ndogo (2500);
b. Awamu ya pili itahusisha utoaji wa shilingi 66,449,000,000.00 kwa wanufaika 4,916 ambao ni vijana (1,416), kampuni za vijana 38, vikundi vya vijana 156 na wafugaji samaki kwa vizimba 3,500; na
c. Awamu ya tatu itahusisha utoaji wa shilingi 84,865,170,249.00 kupitia Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Kiuchumi.

ii) Kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 54,145,896,309.00 kwa wanufaika 11,965 kupitia Mifuko ifuatayo:
a. Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali na Wananchi na Mfuko wa Mzunguko wa Mikoani kupitia SIDO - shilingi 1,085,900,000 kwa wanufaika 265;
b. Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa - shilingi 3,175,000,000 kwa wasanii 1,594;
c. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake - shilingi 337,970,000.00 kwa wanawake 45;
d. Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF Microfinance Fund) -shilingi 14,380,000,000.00 kwa wanufaika 5,573;
e. Mpango wa uwezeshaji wa wafanyabiashara ndogondogo – shilingi 1,534,730,000 kwa wanufaika 709;
f. Mfuko wa mikopo ya asilimia 10 kuwezesha wanawake, vijana, na wenye ulemavu kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri - shilingi 33,454,296,309.00 kwa vikundi 3,776 vya wanawake, vijana na wenye ulemavu; na
g. Mfuko wa *Samia Commercialization Fund* kwa kushirikiana na Benki ya CRDB - shilingi Milioni 667 kwa Kampuni Changa 7.

iii) Kutambuliwa na kurasimisha wafanyabiashara ndogondogo 1,054,149 ambao wamesajiliwa na kupatiwa vitambulisho, nembo, vyeti na leseni za biashara kwa mchanganuo ufuatao:
a. Wafanyabiashara ndogondogo 119,595 (wanawake ni 73,341 na wanaume ni 46,254) wamesajiliwa kupitia Mfumo wa WBN – MIS na kupewa

vitambulisho. Katika ya hao Machinga ni 103,102, Mama na Baba Lishe ni 12,384 na Waendesha Bodaboda na Bajaj 4,109;

b. Wafanyabiashara ndogondogo 30,205 wamesajiliwa kupitia mfumo wa Wezesha portal na kupewa leseni;
c. Wajasiriamali 125,621 wamesajiliwa na kupewa leseni kupitia mfumo wa mfumo wa TAUSI;
d. Waendesha pikipiki na bajaji 209,632 wamerasimishwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) na kupatiwa leseni za udereva;
e. Wafanyabiashara ndogondogo 16,325 wamesajiliwa na kupatiwa leseni ya biashara kupitia SIDO;
f. Wajasiriamali wadogo na wadogo kabisa zaidi ya 3,900 wamepatiwaa namba za mlipa kodi (TIN) na leseni za biashara;
g. Wafanyabiashara 192 wamesajiliwa na kupatiwa Nembo ya ubora na TBS;
h. Wajasiriamali 4,578 (Wavuvi 2,100 na Wafugaji viumbe maji 2,478) wamerasimishwa na kupatiwa vyeti kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi;
i. Vijana 317 wamerasimishwa na kuwezeshwa kuwekeza kwenye miradi ya ufugaji Samaki kwenye vizimba (vijana 164) na vijana 153 kuwekeza kwenye ufugaji wa majongoo Bahari, kilimo cha mwani na unenepeshaji kaa;
j. Vijana 282 (Ke 80, Me 202) wamerasimishwa na kuwezeshwa kufanya kilimo biashara kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (Building A Better Tomorrow – BBT);
k. Wakulima 532,023 (Ke – 171,705 na Me – 360,318) wamesajiliwa na kurasimishwa katika mfumo wa ruzuku ya mbolea;
l. Wachimbaji wadogo 2,239 wamerasimishwa kupitia Wizara ya Madini; na
m. Vikundi 1,216 vya makundi maalum vimesajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA). Kati ya hivyo, vikundi 1,123 vimepata zabuni za ununuzi zenye thamani ya shilingi 31,077,377,783.67 katika miradi ya umma kupitia sheria inayoelekeza asilimia 30 ya manunuzi ya umma kutengwa kwa makundi maalum; na
n. Wafugaji 8,024 wamerasimishwa na kupewa mafunzo ya kilimo cha malisho; uboreshaji wa nyanda za malisho; afya ya mifugo na ya kilo 4,000 za vipando vya malisho kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI);

iv) Kutoa huduma mbalimbali ikiwemo chakula, malazi, elimu na huduma za afya kwa watoto 16,130 wanaoishi katika makao 433 ya Serikali na binafsi; na

v) Kuundwa na kuhuisha majukwaa 15,147 ya wanawake ili kuwawezesha kupata fursa za mikopo pamoja na elimu ya ujasiriamali.

### 10.3. MAENDELEO YA VIJANA

Vijana ni rasilimali muhimu na nguvu kazi katika maendeleo ya jamii na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeunda Wizara ya Maendeleo ya Vijana iliyo Chini ya Ofisi ya Rais ili kusimamia na kuimarisha ustawi wa vijana nchini. Katika kipindi cha utekelezaji, mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo;

i. Kuimarisha ushiriki wa vijana katika utekelezaji wa Ajenda ya Maendeleo ya Taifa kwa kufanya majadiliano ya moja kwa moja na vijana 8,120 katika maeneo ya shughuli za uzalishaji mali katika Mikoa ya Songwe, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Dar es Salaam na Dodoma ili kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili;
ii. Kutenga fedha kiasi cha Shilingi bilioni 8 kwa ajili ya kutekeleza Programu za kipaumbele za Maendeleo ya vijana ambapo jumla ya vijana 1,222 wanatarajiwa kunufaika;
iii. Kuzindua Jukwaa la Vijana (Vijana Platform) jumuishi na shirikishi kwa vijana wa Miji na Vijiji litakalotumika kuchambua masuala yanayohusu ustawi na maendeleo yao; na
iv. Kutoa elimu ya biashara kwa vijana 1,500 na kuwawezesha kujisajili katika mfumo wa Kielektroniki wa manunuzi ya Serikali (TANSIS) kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

### 10.4. KUDHIBITI UZALISHAJI NA USAMBAZAJI WA DAWA ZA KULEVYA

Serikali imeendelea kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa Dawa za Kulevya kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupunguza uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya ikiwemo kuvunja mitandao mikubwa ya usafirishaji na utengenezaji wa dawa za kulevya hivyo kuimarisha ustawi wa jamii kwa ujumla. Vilevile, Serikali imeendelea kuhakikisha mashamba yaliyokua yanatumika kwa kilimo cha bangi na mirungi yanatumika kwa kilimo cha mazao mbadala. Mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

a) Kukamata jumla ya kilogramu 24,716.79 za dawa za kulevya na gramu 141.18 za dawa tiba zenye asili ya kulevya zikihusisha watuhumiwa 1,203 (wanaume 1,079 na wanawake 124). Dawa za kulevya zilizokamatwa ni pamoja na Bangi kilogramu 18,616.065, Skanka kilogramu 620.634, Mirungi kilogramu 4,728.081, Heroin kilogramu 574.029, Cocaine kilogramu 5, Methamphetamine kilogramu 172.8, MDMA

kilogramu 0.178, Flunitrazepam gramu 10.03; Pethidine gramu 104.5, Morphine gramu 4.65 na Fentanyl gramu 22;

b) Kuteketeza ekari 112.8 za mashamba ya bangi 3,495 katika Wilaya ya Tarime (Mara), Wilaya ya Nzega (Tabora), Wilaya ya Makete (Njombe) na Wilaya ya Sengerema (Mwanza). Vilevile, kilogramu 1,030 za mbegu za bangi pamoja na kilogramu 812.46 za dawa za kulevya aina ya mirungi na bangi zimeteketezwa;

c) Kufungua mashauri 260 katika Mahakama mbalimbali nchini kwa kipindi cha kuanzia mwezi Novemba, 2025 hadi Januari, 2026. Vilevile, mashauri 475 ya dawa za kulevya yanayoendelea katika Mahakama mbalimbali nchini yameendelea kufuatiliwa ambapo mashauri 230 yametolewa hukumu na Jamhuri imeshinda mashauri 172; na

d) Kutoa tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya 4,790 (wanaume 4,610, wanawake 180) waliopo kwenye kliniki 18 nchini na waraibu 1,180 (wanaume 1,086, wanawake 94) waliopo kwenye nyumba za upataji nafuu 77.

## 10.5. MAPAMBANO DHIDI YA VVU NA UKIMWI

Serikali imeendelea kuimarisha huduma za udhibiti wa VVU na UKIMWI kwa kuongeza upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji endelevu wa mwitikio dhidi ya VVU na UKIMWI nchini. Hadi kufikia tarehe 28 Januari, 2026 Mfuko wa *Aids Trust Fund* umepokea kiasi cha shilingi bilioni 16.8. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa za magonjwa nyemelezi kwa WAVIU (shilingi bilioni 8.40 sawa na asilimia 50); kutekeleza afua za Kinga (shilingi bilioni 7.90 sawa na asilimia 47); na kutekeleza shughuli za usimamizi na uratibu wa mfuko (shilingi bilioni 0.50 sawa na asilimia 3).

## 10.6. URATIBU WA SHUGHULI ZA MAAFA

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i). Ununuzi wa boti mbili za kupambana na uharamia katika bahari na maziwa makuu. Boti hizo zitaimarisha usalama wa wananchi wanaotegemea shughuli za uvuvi na usafiri wa majini katika bahari na maziwa makuu. Boti hizo zitachangia kupunguza matukio ya uharamia na uhalifu; kuokoa maisha wakati wa dharura; kulinda mali za wananchi; na kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika maeneo ya bahari na maziwa makuu kwa mazingira salama; na

ii). Kuandaa miongozo ya uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya dharura na timu za utayari za kukabiliana na dharura ngazi ya mkoa. Miongozo hiyo itasaidia kuanzisha

na kuendesha vituo vya dharura na timu za utayari katika mikoa yote nchini na hivyo kuongeza ufanisi katika kukabiliana na maafa nchini.

## 10.7. HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Serikali inatambua umuhimu wa Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kuhabarisha umma, kuhifadhi mila na desturi pamoja na kuhamasisha ushiriki wa wananchi hususani vijana katika michezo na utamaduni hivyo kuzalisha ajira na kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hiyo ni pamoja na:

i. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya michezo kwa ajili ya mashindano ya AFCON 2027 ikiwemo ujenzi wa uwanja wa mpira wa Arusha ambao umefikia asilimia 74 na ukarabati viwanja vya Benjamin Mkapa umefikia asilimia 95 na Uhuru asilimia 70;

ii. Kuiwezesha Timu ya Taifa (Taifa Stars) kushiriki katika mashindano ya AFCON 2025 yaliyofanyika nchini Morocco ambapo Taifa Stars iliweka historia kwa kufanikiwa kufika hatua ya 16 bora katika mashindano hayo;

iii. Kukamilika kwa ujenzi na kuanza kutoa huduma kwa kituo cha redio masafa ya FM katika Mji wa Itigi.

## SURA YA KUMI NA MOJA

### 11. HITIMISHO

Mafanikio yaliyopatikana katika siku 100 za utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yameonesha dhamira halisi ya kuleta maendeleo kwa wananchi na kasi kubwa ya utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyoahidiwa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Serikali itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa kuendelea kujenga miundombinu ya utoaji wa huduma za jamii, usafiri na usafirishaji; kutatua kero za wananchi; kuimarisha mahusiano ya ndani na nje ya nchi; pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi ili kufikia mipango ya Kitaifa ikiwemo Dira 2050 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.